

Jina ..... Namba yako.....

Sahihi ya matahiniwa .....

Tarehe .....

**102/2**

**Karatasi ya Pili**

**LUGHA**

**JULAI/ AGOSTO 2013**

**MUDA: SAA 2<sup>1</sup>/<sub>2</sub>**

**TATHMINI YA PAMOJA YA WILAYA YA LAIKIPIA  
(LENOCET) MWAKA WA 2013  
CHETI CHA KUHITIMU ELIMU YA SEKONDARI**

**102/2**

**Karatasi ya Pili**

**LUGHA**

**MUDA: SAA 2<sup>1</sup>/<sub>2</sub>**

**MAAGIZO**

- (a) Andika jina lako na namba yako ya mtihani katika nafasi ulizowachiwa hapo juu.
- (b) Tia sahihi yako kisha uandike tarehe ya mtihani katika nafasi ulizowachiwa hapo juu.
- (c) Jibu maswali yote.
- (d) Majibu yako yaandikwe katika nafasi ulizoachiwa katika kijitabu hiki cha maswali.
- (e) Usitoe ukurasa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
- (f) Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote za karatasi hii zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**Kwa matumizi ya matahini pekee.**

<b>SWALI</b>	<b>UPEO</b>	<b>ALAMA</b>
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
<b>JUMLA</b>	<b>80</b>	

## 1. UFAHAMU

### **Soma makala yafuatayo kisha ujili maswali.**

Mwanamke wa kisasa anazaliwa na kukulia katika mazingira yaliyobadilika mno. Matazamio yake maishani ni tofauti kabisa na yale ya wanawake walioishi mapote mawili yaliyopita; wanawake makamu ya nyanyake na mamake-kuu.

Yeye hatarajii kuzaliwa, kukua, kuolewa, kuwa mke wa bwana, kumzalia mumuwe watoto na daima dawamu kuwa 'mwendani wa vijungu jikoni' akawapikia watoto na bwanake chakula; na akitoka jikoni aelekee shambani kulima, kichakani kuchanja kuni, mtoni kufua nguo na kuteka maji ya kutumianyumbani. Mwanamke wa kisasa huandamana na mwanamume. Akanyagapo mume, naye papo huutia wayo wake.

Mwanamke wa kisasa huenda shule na kujifunza yote yafunzwayo huko. Hushindana na wanwake kwa wanaume na kuibuka mshindi si mara haba. Huibuka mshindi katika masomo ya lugha, historia, jiografia, hesabu, sayansi na mengineyo, sawa na mwanamume.

Mwanamke wa kisasa hutaka kufanya kazi ya kibega, akazifanya. Akataka kuwa mwalimu, akawa. Akataka kuwa daktari, akafanikiwa. Almuradi, siku hizi mwanamke hufanya kazi yoyote ile afanyayo mwanamume. Kuna wanawake marubani wa ndege, masonara, waashi, wahandisi, madereva wa magari, mawakili, mahakimu, mawaziri wakuu na hata marais wa nchi. Hakuna kazi isiyofanywa na mwanamke siku hizi.

Mwanamke wa kisasa hateswi akafyata ulimi. Anapohiniwa yeye hupigania haki yake kwa dhati na hamasa. Katu hakubali 'mahali pake' katika jamii alipotengewa na wanaume wenye mawazo ya kihafidhina yaliyopitwa na wakati.

Siku hizi mwanamke huolewa tu wakati amepata kazi ya kumwezesha kujikimu maishani au pale anapokuwa na hakika kwamba biashara yake, iwapo ni mfanyi biashara, imepiga hatua ya kutomrudisha ukatani.

Mwanamke wa kisasa haamuliwi katika jambo lolote, bali hufanya maamuzi yake mwenyewe. Kwa upande mwagine, mwanamume wa '*kisasa*' ambaye bado amefungwa pingu na taasubi za kiume, hapendezwi na mwanamke huyu. Huuma kidole akatamani ya kale, lakini wapi! Analazimika kumkabili mwanamke huyu kama mshirika sawa maishani na kuishi naye, apende asipende. Shingo upande analazimika kukubali kwamba mabadiliko haya sio mithili ya kiwingu kipitacho, bali ni ya aushi.

### **Maswali**

- (a) Msemo '*mwendani wa vijungujiko*' unadhihirisha hali gani ya mwanamke katika jamii? (alama 2)

---

---

- (b) Jamii imefanya mwanamke kuwa hayawani wa mzigo. Fafanua. (alama 1)

---

---

- (c) Eleza maana ya '*akanyagapo mume, naye papo huutia wayo wake.*' (alama 1)

---

---

- (d) Zungumzia maswala ya ndoa na elimu hukuzukilinganisha mwanamke wa kiasili na wa kisasa. (Alama 4)

---

---

---

---

---

---

- (e) Mwanamume wa kisasa anamwonaje mwanamke wa kisasa? (Alama 1)

---

---

- (f) Taja mifano mitatu ya mawazo ya kihafidhina. (Alama 3)

---

---

---

---

---

---

- (g) Eleza maana ya; (Alama 3)

(i) Akafyata ulimi

---

(ii) Ukatani

---

(iii) Aushi

---

## **2. UFUPISHO**

Ajira ya watoto ni tatizo sugu linalokumba ulimwengu wa sasa, hasa katika nchi zinazoendelea. Jambo lakusikitisha ni kwamba hivi ndivyo vilivyo, katika nchi nyngi za ulimwengu huu. Kuna idadi kubwa ya watoto wanaoajiriwa katika nyanja mbalimbali za jamii. Zipo sababu nyngi zinaowasukuma watoto kutafuta ajira barani Afrika kwa mfano, familia nyngi huishi maisha ya ufukara hivi kwamba hushindwa kuyatimiza mahitaji muhimu hususan kwa watoto. Kupanda kwa gharama ya maisha kunazidisha viwango vya umaskini. Ukosefu wa lishe pia huwfanya watoto kutoroka nyumbani kutafuta ajira. Janga la UKIMWI limesababisha kuwepo kwa idadi kubwa ya mayatima wanaoishia kutafuta ajira ili kuyakimu maisha. UKIMWI umezifanya familia nyngi pia kuwaondoa watoto shulen iili wawze kuajiriwa kwa lengo la kualisha pato la familia hizo.

Wengine huijingi za katika vitendo vya jinai pale wanapokosa ajira. Huchukua sheria mikononi mwao, wakaendeleza vitendo vya uktili kama vile kuwahangaisha watu na kupora mali yao au hata kuwakaba roho. Aidha, wengine hujikuta kwenye madanguro ambako huendesha biashara haramu.

Uundaji wa umoja wa Afrika hivi majuzi ni hatua muhimu ya kushughulikia matatizo ya Afrika kama vile ajira ya watoto, kuzorota kwa miundo msingi, magonjwa, njaa, umaskini, ufisadi na ukabila. Katika kushughulikia hali za watoto nchi za Afrika hazina budi kuzingatia masharti yaliyowekwa na umoja wa mataifa kuhusu haki za watoto. Nchi nyngi za Afrika ziliidhinisha mkataba wa masharti hayo ikiwemo nchi ya Kenya. Nchi hizi basi lazima zishughulikie haki za watoto kuititia sheria za nchi. Watoto ni rasilimali muhimu na ndipo tumaini la kuwepo kwa kizazi cha binadamu.

### **Maswali**

- (a) Eleza mambo yote muhimu anayozungumzia mwandishi katika aya ya kwanza.  
(Maneno 45 - 50) (Alama 7, 1 ya utiririko)

### **Matayarisho**

---

---

---

---

---

---

### **Jibu**

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

- (b) Fupisha aya mbili za mwisho (maneno 50-55) (Alama 8, 1 ya utiririko)

## Matavarisho

Jibu

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

### 3. MATUMIZI YA LUGHA: (Alama 40)

- (a) (i) Eleza maana ya kiambishi. (alama 1)

---

---

- (ii) Onyesha viambishi tamati katika vitenzi vifuatavyo. (alama 2)

Ambaye

---

---

Aishiko

- (b) Eleza matumizi ya 'ka' katika sentensi hii. (alama 1)

Kachezeni nje!

---

---

- (c) Andika vitamkwa vyenye sifa zifuatazo vinapotamkwa. (alama 2)

- (i) Midomo wazi

---

---

- (ii) Midomo kuviringwa

---

---

- (d) Tumia kiwakilishi cha -a unganifu kutunga sentensi katika ngeli ya KU - KU. (alama 1)

---

---

- (e) Andika sentensi ifuatayo katika wakati ujao hali timilifu: (alama 1)

Lugha ya kiswahili ilienea Afrika kote.

---

---

- (f) Changanua sentensi ifuatayo kwa kutumia kielezo cha matawi. (alama 4)

Wanafunzi walimaliza kazi yote kisha wakaenda nyumbani.

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

- (g) Tungia kitawe ‘*pasi*’ sentensi mbili kuboaa maana tofauti za neno hili. (alama 2)

---

---

---

- (h) Bainisha vielezi na ueleze ni vya aina gani katika sentensi hii. (alama 2)  
Sipendi wanaohama kwao ili kuenda kuishi kizungu.

---

---

---

- (i) Tumia kauli za vitenzi kulingana na maagizo. (alama 2)  
Paka (kauli ya kutendata)

---

---

Ficha (kauli ya kutendama)

---

---

- (j) Akifisha sentensi ifuatayo: (alama 3)  
rais alimwamuru usiwashughulikie mabalozi wajeuri.

---

---

---

- (k) Eleza matumizi ya maneno haya: (alama 2)  
Anapendezwa na kucheza kule.

---

---

---

Jioni mtaenda kucheza.

---

---

- (l) Kanusha sentensi hii. (alama 2)  
Nilimwona rafiki yako na nikamwambia kuwa ulimsalimu.

---

---

- (m) (i) Eleza maana ya kiimbo. (alama 1)  
\_\_\_\_\_  
  
(ii) Onyesha kiimbo kiwezayo kutokea katika neno hili.  
'amekusamehe'  
\_\_\_\_\_
- (n) Andika neno moja lenye maana sawa na taadhima. (alama 1)  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (o) Bainisha aina za vishazi katika sentensi. (alama 2)  
Wakilipa deni la mkopo watarejeshewa mali yao.  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (p) Andika katika usemi halisi. (alama 3)  
Mama alinionya kuwa nilimokuwa nikichezea mlikuwa na hatari.  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (q) Weka sentensi hii katika udogo hali ya wingi. (alama 2)  
Guu lake lilipona baada ya kuumwa na jibwa.  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (r) Ainisha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (alama 2)  
Mwalimu alisoma barua aliyandikiwa mwanafunzi.  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_
- (s) Eleza maana mbili za sentensi hii; (alama 2)  
Lo! Amenikimbilia.  
\_\_\_\_\_  
\_\_\_\_\_

**4. ISIMU JAMII**

“Nataka kuunga mkono waziri mwenye kangu katika mswada huu wa kupiga marufuku unywaji wa pombe haramu..... Bwana Spika .....

- (a) Tambua sajili hii. (alama 2)

---

---

---

---

- (b) Huku ukitoa mifano, eleza sifa za sajili hii. (alama 8)

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---